# ASOMAYE NA AFAHAMU….
## Na Willy Emmanuel Yudah

**Karibu mpenzi msomaji katika jarida la "Asomaye na Afahamu". Leo nitajikita katika mada inayozungumzia uwepo wa Mungu. Wapo watu ambao hawaamini kwamba Mungu Yupo. Bahati mbaya hata baadhi ya wale wanaoenda kanisani wana wasiwasi na kuwepo kwa Mungu. Karibu….**

## MUNGU

*"Hapo mwanzo Mungu aliumba mbingu na nchi" Mwanzo 1:1.*

Huu ndiyo mstari wa kwanza kabisa katika Biblia.

Vitu vyote huanza na Mungu,
Biblia huanza na Mungu,
Tunapojifunza Biblia lazima tuanze na Mungu, maana Biblia ndicho kitabu chake.

**"Mungu yukoje?" "Tunawezaje kujua kwamba Mungu yupo?"**
Haya ni maswali muhimu ambayo kila mtu anaweza kuuliza. Hakuna lililo muhimu kuliko majibu ya maswali haya. Majibu ya maswali haya yataamua tunavyotakiwa kuishi tuwapo hapa duniani. Majibu ya maswali haya yataamua tutakakoishi baada maisha ya hapa duniani. Tufungue Biblia, Kitabu cha Mungu, ili kuona majibu.

## 1. MUNGU YUKOJE?

Mungu ni wa milele!
Amekuwepo muda wote na atakuwepo muda wote. Kuhusiana na Mungu, Biblia inasema;

*"Kabla haijazaliwa milima, wala hujaimba dunia,*
*Na tangu milele na milele wewe ndiwe Mungu." Zaburi 90:2.*

Wanadamu wote waishio duniani watazeeka. Sote tutakufa. Lakini Mungu hazeeki wala hafi. Ona Biblia inavyosema tena;

*"Hapo Mwanzo uliutia msingi wa nchi, Na mbingu ni kazi ya mikono yako.*
*Hizi zitaharibika, bali wewe utadumu, Naam, hizi zitachakaa kama nguo;*
*Na kama mavazi utazibadilisha, nazo zitabadilika. Lakin wewe U Yeye yule;*
*Na miaka yako haitakoma." Zaburi 102:25-27, Waebrania 1:10-12.*

Mungu ni muweza!

*"Kuna neno gani gumu la kumshinda BWANA?" Mwanzo 18:14.*

Sisi wanadamu ni wanyonge. Kuna mambo mengine hatuwezi kufanya kutokana na kukosa nguvu. Walakini Mungu ni muweza wa yote. Anaweza kufanya lolote. Kwa uweza wake mkuu, Mungu aliziumba mbingu na nchi. Kwa uweza wake mkuu, Mungu alimuumba mwanadamu. Tunaweza kuziamini ahadi za Mungu. Ana uweza kuzitimiza.

Mungu anafahamu yote!

Mungu anafahamu kila kitu kwa sababu anaona kila kitu. Unaweza kuwaficha kitu wanadamu, lakini kwa Mungu hakuna linaweza kifichika! Hebu tazama…

*"Kwa maana njia za mwanadamu zi mbele za macho ya BWANA,*
*Na mienendo yake yote huitafakari" Mithali 5:21*

*"Kwa maana Mungu ni mkuu kuliko mioyo yetu" 1 Yohana 3:20*

Mungu habadiliki na wala si kigeugeu!

Hapa duniani kila kitu hubadilika, hata watu hubadilika. Tabia na desturi za watu hubadilika, hali ya hewa hubadilika, mitindo hubadilika na hata miili yetu wenyewe hubadilika kadri tunavyokua.

*"Kwa kuwa mimi, BWANA, sina kigeugeu;" Malaki 3:6*

Mungu ni Roho!

Mungu si mwanadamu kama vile mimi na wewe tulivyo.

*"Mungu ni **<u>Roho</u>**, nao wamwaduo yeye imewapasa kumwabudu katika roho na kweli"*

Mungu hana udhaifu na magonjwa ya mwili kama mimi na wewe tulivyo.

*"Kwa kuwa roho haina **<u>mwili na mifupa</u>** ….." Luka 24:39*

Mungu ni nuru!

*"Na hii ndiyo habari tuliyoisikia kwake, na kuihubiri kwenu, ya kwamba **Mungu ni nuru,** wala giza lolote hamna ndani yake" 1 Yohana 1:5.*

Ndani ya Mungu hakuna giza (dhambi). Kwa sababu hii, twaweza kumwamini maana hawezi kusema uongo (kutupotosha).

Mungu ni Upendo!

*"Yeye asiyependa, hakumjua Mungu, kwa maana **<u>Mungu ni upendo."</u>** 1Yohana 4:8*

Mungu anatupenda. Aliudhihirisha upendo wake kwetu kwa kumtoa mwanawe kufa kwa ajili ya dhambi zetu-kifo cha msalaba!

*"Hili ndilo pendo, si kwamba sisi tulimpenda Mungu, bali kwamba yeye alitupenda sisi, akamtuma mwanawe kuwa kipatanisho [*kulipa fidia-kifo cha kunyongwa msalabani*]kwa dhambi zetu" 1Yohana 4:10*

Mungu ni mtakatifu!

*"Mtakuwa watakatifu; kwa kuwa mimi BWANA,* ***Mungu wenu, ni mtakatifu****" (Walawi 19:2*

Mungu ni mwenye haki!
Hawezi kukosea. Anachukia dhambi zote.

*"Kwa kuwa BWANA ndiye mwenye haki,*
*apenda matendo ya haki,*
*wanyofu wa moyo watamwona uso wake."Zaburi 11:7*

Mungu ana huruma!
Mungu anatupenda. Ingawaje anaichukia dhambi lakini ana huruma. Atausamehe dhambi zetu endapo tutazitubia kwelikweli. Twasoma,

*"BWANA amejaa huruma na neema,*
*Haoni hasira upesi, ni mwingi wa fadhili" Zaburi 103:8*

**TUNAJAUJE KWAMBA MUNGU YUPO?**

Twajua ya kwamba Mungu yupo kwa sababu ya kuona vitu alivyoviumba, ndiposa twasoma,

*"Mbingu zahubiri utukufu wa Mungu,*
*na anga laitangaza kazi ya mikono yake" Zaburi 19:1.*

Tukiiona nyumba twafahamu kuwa kuna fundi aliyeijenga. Nyumba haiwezi kuwepo bila fundi washi kuwepo. Katika namna iyo hiyo, tuonapo jua, mwezi, nyota, dunia, na vyote vilivyomo twajua kwamba yupo aliyevitengeneza. Mungu pekee ana uwezo wa kuzifanya mbingu na nchi. Kwa hiyo, tunajua Mungu yupo pindi tunapoona vitu alivyovifanya.

Tunafahamu kuwa Mungu yupo kwa sababu dhamiri zetu zetu zinatuambia hivyo. Wanadamu wana hali kuamini uwepo wa nguvu fulani kuu. Jambo hili limekuwepo tangu kale katika mioyo ya watu katika kila taifa na zama. Watu wamekuwa wakimwamini Mungu na wengine kwa dhana isiyo sahihi. Twasoma,

*"Kwa maana watu wa mataifa wasio na sheria wafanyapo kwa tabia zao yaliyo ndani ya torati, hao wasio na sheria wamekuwa sheria kwa nafsi zao wenyewe……"Warumi 2:14-16*

Twajua ya kwamba Mungu yupo kwasababu amejifunua mwenyewe katika Kristo Yesu; Basi twasoma,

> *"Mungu ambaye alisema zamani na baba zetu katika manabii kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi, mwisho wa siku hizi amesema na sisi katika Mwana, aliyemweka kuwa mrithi wa yote, tena kwa yeye aliufanya ulimwengu" Waebrania 1:1-2*